



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتُخْفَنُهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُكَفِّرُوهُمْ اللَّهُ أَرْضُنَا هُمْ وَلَيَسْبِلَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَقِيقَتِهِمْ أَمَّا  
يَعْبُدُونَ فَلَا يُشْرِكُونَ بِإِلَهٍ مُّنَاهٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Toleo: 1444 / 02

Jumatano, 9 Rabi' I 1444 H

05/10/2022 M

### Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

[من المؤمنين رجال صدقو ما عاهدوا الله عليه فمنهم من قضى نحبه ومنهم من ينتظر وما بدلوا تبديلا]

"Mionganoni Mwa Waumini Wapo Waliotimiza Waliyoahidiana Na Mwenyezi Mungu. Baadhi  
Yao Wamekwisha Kufa, Na Baadhi Wanangojea, Wala Hawakubadilisha (Ahadi) Hata  
Kidogo." [Al-Ahzaab: 23]

(Imetafsiriwa)

Hizb ut Tahrir / Tanzania inaombeleza kifo cha mlinganizi wake kijana kwa jina Abdi Gibu Barie (38) wa mkoani mwanza, Kaskazini Magharibi ya Tanzania.

Amerejea kwenda kwenye rehma ya Mwenyezi Mungu (swt) mnamo siku ya Jumatatu, 03 Oktoba 2022 miladi sawa na tarehe 08 Rabi' al-Awwal 1444 Hijria.

Abdi Gibu Barie (Mwenyezi Mungu airehemu roho yake), licha ya kuwa alikuwa bado mwanafunzi (katika Hizb) alikuwa mmoja kati ya wanaharakati thabiti mwenye bidii na mwenye muhanga wa hali ya juu katika da'awa ya kurejesha tena maisha ya Kiislamu, kiasi kwamba hata katika muda wake wa mwisho katika uhai wake, ndani ya siku ya Jumapili 02 Oktoba 2022 alishiriki kikamilifu katika amali za Hizb.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kummiminia marehemu katika rehma zake zilizoenea, amsamehe na kumpokea katika Pepo yake yenye wasaa. Pia (sisi Hizb) tunaungana katika maombolezo haya na familia, ndugu na marafiki (wa marehemu), huku tukiomba kwa Mwenyezi Mungu Subhanahu Wa Ta'ala kutupa sisi nao wao subra na faraja ya hali ya juu.

[إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِفُونَ]

"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na hakika kwake Yeye tunarejea" [Al-Baqarah:156]

Masoud Msellem  
Mwakilishi kwa Vyombo vy ya Habari  
Hizb ut Tahrir Tanzania